**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI**
**(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**

**MKOA WA KILIMANJARO**
Simu : 27-29 74369
Fax : 27- 29 74368
Email: ded@haidc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya Hai,
3BR-TTCL-Kanisani,
25382. Bomang'ombe,
S.L.P. 27,
**HAI KILIMANJARO**

Kumb.Na. LG/F.20/70/85

Tarehe: 19/12/2024

Kwa Watumishi wote wa
Halmashauri ya Wilaya ya Hai.

## TANGAZO LA MKOPO

Mkurugenzi Mtendaji anawatangazia Watumishi wote kuwa ofisi ya Katibu Mkuu Hazina imetoa Mgao wa fedha za mikopo kwa Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya wa Hai ili watumishi waweze kuomba. Maombi ya mkopo yanafanyika kwa njia ya mtandao (Online Loan Application), hivyo Watumishi wote wenye uhitaji wa mkopo muwasilishe maombi yenu kwenye mfumo wa mikopo ya Hazina (ALS).

Maombi yote yawasilishwe kwenye mfumo kuanzia tarehe 19/12/2024 hadi tarehe 27/12/2024.

Masharti ya Mkopo;-

1. Kiasi cha Mkopo kinachoombwa ni lazima kizingatie ngazi ya Mshahara.
2. Makato ya Mkopo yazingatie salio la 1/3 ya mshahara.
3. Mwombaji awe ni Mtumishi aliyethibitishwa kazini.
4. Mtumishi ambaye tayari ana mkopo wa Hazina na bado anadaiwa haruhusiwi kuomba.
5. Mkopo ni lazima uwe kwa ajili ya ununuzi wa gari, pikipiki, samani na matengenezo ya gari la Mtumishi.

Maelekezo ya namna ya kujisajili na kuomba mkopo yanapatikana kwenye manual ambayo imeambatanishwa na tangazo hili.

Tangazo hili limetolewa leo tarehe 19/12/2024.

Dionis M. Myinga
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**HAI**

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR